HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE

14 - 15/02/2018

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Mhe. Juma A. Kimisha - Diwani Kata ya Nyamilangano- **Mwenyekiti**
2. Mhe. Gagi Lala Gagi - Diwani Kata ya Igwamanoni – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Tabu R. Katoto - Diwani Kata ya Igunda
4. Mhe. Yohana E. Mange - Diwani Kata ya Mapamba
5. Mhe. Emmanuel N. Makashi - Diwani Kata ya Sabasabini
6. Mhe. Mabala K. Mlolwa - Diwani Kata ya Chona
7. Mhe. Yuda L. Majonjos - Diwani Kata ya Idahina
8. Mhe. Mkomba P. Daudi - Diwani Kata ya Ukune
9. Mhe. Kulwa D. Shoto - Diwani Kata ya Bukomela
10. Mhe. Bundala J. Christopher - Diwani Kata ya Uyogo
11. Mhe. Benedicto A. Mabuga - Diwani Kata ya Mpunze
12. Mhe. Pili E. Sonje - Diwani Kata ya Ushetu
13. Mhe. Sharifu A. Samwel - Diwani Kata ya Kinamapula
14. Mhe. Paschal N. Mayengo - Diwani Kata ya Ulowa
15. Mhe. Doa M. Limbu - Diwani Kata ya Nyankende
16. Mhe. Kulwa E. Mabula - Diwani Kata ya Ulewe
17. Mhe. Damas J. Njige - Diwani Kata ya Chambo
18. Mhe. Hamis M. Majogoro - Diwani Kata ya Ubagwe
19. Mhe. Joseph M. Masaluta - Diwani Kata ya Bulungwa
20. Mhe. Golani P. Sayi - Diwani Kata ya Kisuke
21. Mhe. Gabriela A. Kimaro - Diwani Viti Maalum
22. Mhe. Bernadetha M.Jumanne - Diwani Viti Maalum
23. Mhe. Mary I. Lundalila - Diwani Viti Maalum
24. Mhe. Bether L. Bugaywa - Diwani Viti Maalum
25. Mhe. Esther M. Imambo - Diwani Viti Maalum
26. Mhe. Felister N. Kabasa - Diwani Viti Maalum
27. Mhe. Eva P. Mkonya - Diwani Viti Maalum
28. Ndg. Michael Matomora - Mkurugenzi Mtendaji (W) – **Katibu**

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

1. Mhe. Elias J. Kwandikwa - Mbunge Jimbo la Ushetu – kwa taarifa

WATAALAM WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Manyama Katikiro - Kaimu Afisa Utumishi (W)

2. Ndg. Gervas Magogozwa - Afisa Utamaduni (W)
3. Ndg. Minael Ngomoi - Afisa Maendeleo ya Jamii
4. Ndg. Kawishe Lucas - Afisa Ufugaji Nyuki (W)
5. Ndg. Onesmo Benjamin - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
6. Ndg. Anna Ngongi - Afisa Kilimo na Ushirika (W)
7. Ndg. Deus Kakulima - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
8. Ndg. Alfred Rukelegwa - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
9. Ndg. Morgan Mwita - Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI
10. Ndg. Khadija Ismail - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
11. Ndg. Marco Mwairwa - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
12. Ndg. Given Ngilangwa - Kaimu Afisa Ushirika (W)
13. Ndg. Selestine Lufundisha - Afisa Biashara (W)
14. Ndg. Godfrey Lwambula - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
15. Ndg. Neuster James - Mwanasheria (W)
16. Ndg. Athanas Lucas - Afisa Usafi na Mazingira (W)
17. Ndg. Tumshukuru C. Mudui - Afisa Tarafa Dakama
18. Ndg. Edith Mpinzile - Afisa Elimu Msingi (W)
19. Ndg. Sadick Mwita - Afisa Ugavi na Manunuzi (W)
20. Ndg. Stephano B. Kaliwa - Mhandisi wa Maji (W)
21. Ndg. Salakana J. Peter - Afisa Tarafa Mweli
22. Ndg. Aston Mnkeni - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
23. Ndg. Samwel Uroki - Kaimu Afisa Mipango (W)
24. Ndg. Noela Masawe - Kaimu Mganga Mkuu (W)
25. Ndg. Denis Jamhuri Pius - Mratibu wa TASAF III
26. Ndg. Ephraim Kaijuko - Mthibiti Ubora wa Shule – KAHAMA
27. Ndg. Valentina Majembe - Afisa Utumishi - TSC

WAGENI WAALIKWA WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Bakari Ndee - Kny: Mkuu wa Magereza (W)
2. Ndg. Mtua Hassan - Kny: Afisa Usalama (W)
3. Ndg. Frank Elophacy - Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto
4. Ndg. Henry Mwala - Afisa Uhamiaji (W)
5. Ndg. Mrisho S. Madudi - Kny: Mshauri wa Mgambo (W)
6. Ndg. Lucas Sanya - Afisa TAKUKURU
7. Ndg. Salvatory Given - Mwandishi wa Habari - Kahama FM
8. Ndg. Nyamiti A. Nyamiti - Mwandishi wa habari - Divine FM
9. Ndg. Raymond Mihayo - Mwandishi wa Habari - DailyNews
10. Ndg. Paul Kayanda - Mwandishi wa Habari - Uhuru News
11. Ndg. Alexandarina N. Katabi - Katibu wa Chama cha Mapinduzi (W)
12. Ndg. Fabian M. Kamoga - Afisa Serikali za Mitaa
13. Ndg. Timothy Ndanya - Katibu Tawala (W)
14. Ndg. Shaban Njia - Mwandishi wa habari - Nipashe
15. Ndg. Simon Dioniz - Mwandishi wa habari Kwizera FM

SEKRETARIETI

1. Ndg. Warda Yusuph - Mwandishi wa Vikao (CC)
2. Ndg. Emmanuel Stambuli - Mwandishi Vikao (CC)

MUHT NA. BM/39/2017/2018 - KUFUNGUA MKUTANO

Katibu aliwakaribisha wajumbe, wataalam, wageni waalikwa na Waandishi wa Habari katika mkutano huo, kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kuongoza Dua ya Kuiombea Halmashauri, baada ya Dua hiyo alimkaribisha mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, wataalam, wageni waalikwa na Waandishi wa Habari katika mkutano huo, alieleza kuwa mkutano huo wa Baraza utafanyika kwa siku mbili na kusema kuwa ana imani na wajumbe wa baraza hilo kuwa watafanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu.

Alifungua kikao saa 4:43 asubuhi

MUHT NA. BM/40/2017/2018 - KURIDHIA AJENDA ZA MKUTANO

Katibu aliwasilisha mapendekezo ya ajenda kumi na mbili (12) ili zijadiliwe kwenye mkutano huo kama ifuatavyo:-

TAREHE 14/02/2018

1. Kufungua mkutano
2. Kuridhia ajenda za mkutano
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 06-07/11/2017
4. Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 06-07/11/2017
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi kinachoishia mwezi Desemba, 2017
6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ngazi ya kata
7. Kusitisha mkutano wa Baraza siku ya kwanza

TAREHE 15/02/2018

8. Kurejea kwa mkutano wa Baraza siku ya pili
9. Maswali ya papo kwa papo
10. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili mwaka 2017
11. Taarifa za Kamati za kudumu za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri katika kipindi cha robo ya Pili, Oktoba hadi Desemba, 2017
    a) Kamati ya kudhibiti UKIMWI
    b) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    c) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    d) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
12. Kufunga mkutano

Baada ya kuwasilisha ajenda hizo Mhe. Esther Matone alieleza kuwa katika mtiririko wa ajenda hajaona ajenda ya kukabidhi majengo yaliyopo Kahama Mjini ambayo yalikuwa yakitumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

Katibu Tawala (W) alieleza kuwa tarehe 29 Novemba hadi 01 Desemba kulikuwa na ugeni wa ujio wa Naibu Waziri wa TAMISEMI ambapo alitoa maagizo ambayo yalikuwa ni ya Serikali kuwa moja ya kazi aliyokuja kufanya Mkoa wa Shinyanga ni kukabidhi majengo yaliyokuwa yakitumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu yaliyopo mjini Kahama kwa Halmashauri ya Kahama. Makabidhiano yaliyofanyika hapakuwa na wawakilishi wa wananchi kwa pande zote mbili, hivyo alimuomba Mkurugenzi Mtendaji kuandaa taarifa ya majengo hayo na kutoa taarifa kwa wawakilishi wa wananchi.

Wajumbe walijadili na kueleza kuwa walichohitaji ni ushirikishwaji na kupewa taarifa ya mali iliyokuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na kukabidhiwa kwa Halmashauri ya Kahama Mji.

Mkurugenzi Mtendaji aliomba muda kwa ajili ya kuandaa taarifa ya kukabidhi majengo hayo kisha kuwasilisha kwenye Mkutano wa Baraza linalofuata.

Baada ya majadiliano hayo, wajumbe waliridhia kujadili agenda zote kama zilivyowasilishwa na Katibu.

MUHT NA. BM/41/2017/2018 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 06-07/11/2017

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari huo wa mkutano wa Baraza la madiwani ukurasa kwa ukurasa, mara baada ya kupitia, wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo ni sahihi, Mwenyekiti na katibu walitia saini kwa ajili ya kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

MUHT NA. BM/42/2017/2018 - YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 06-07/11/2017

Majibu ya utekelezaji wa yatokanayo yaliwasilishwa kama ifuatavyo:

Kutoka Muht Na. BM/38/2017/2018 kuhusu muongozo wa Mabaraza yanayoshughulikia ardhi katika ngazi za vijiji na kata.

Azimio kwamba, Wajumbe waliomba Mabaraza yanayoshughulikia ardhi katika ngazi za vijiji kupewa muongozo kwa ajili ya kuendesha mabaraza.

Utekelezaji; Baadhi ya Mabaraza ya vijiji yamepewa mwongozo wa uendeshaji wa mabaraza ya kata kupitia watendaji wa kata.

Utaratibu wa kugawa miongozo hiyo kupitia Watendaji wa Kata unaendelea

Baada ya majibu ya utekelezaji kuwasilishwa, Mhe. Ester Matone na Mhe. Benedicto Mabuga walieleza kuwa utoaji wa miongozo hiyo unasuasua kutokana na maeneo mengine kuwa hayana miongozo, hivyo walitaka kujua utaratibu unaotumika katika kutoa miongozo hiyo. Aidha, kutokana na baadhi ya Kata kupewa miongozo hiyo na

kata zingine kutopewa walishauri Halmashauri ichukue jukumu la kuwakutanisha watendaji wa kata na kuwapa mafunzo ya pamoja na kukabidhi miongozo hiyo.

Mwanasheria alieleza kuwa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango iliagiza kuvunja mabaraza yaliyopita na kuunda Mabaraza mapya ambayo yatapewa mafunzo na miongozo, hivyo ilielekezwa kuandaa barua na kupeleka katika kata kwa ajili ya kuteua wajumbe ambao wataunda Mabaraza mapya.

Wajumbe kwa pamoja walijadili na kutoa agizo kuwa kwa kuwa Mabaraza hayo muda wake umeisha yavunjwe na kuundwa Mabaraza mengine yatakayopewa mafunzo na miongozo kwa ajili ya kuongoza Mabaraza hayo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa amepokea ushauri uliotolewa na wajumbe, hivyo aliomba kuchukua suala hilo na kwenda kuchakata, kwa kusitisha Mabaraza yaliyopo, kuunda mapya, kutoa mafunzo na kutoa muongozo ili yaanze kufanya kazi na taarifa kuwasilishwa katika Mkutano wa Baraza litakalofuata.

Kutoka Muht Na. BM/38/2017/2018 Kuhusu *"power tiller"* zilizonunuliwa na Halmashauri

Azimio Kwamba; Kwa kuwa *"power tiller"* zilinunuliwa wakati Halmashauri haijagawanywa na zilikabidhiwa katika vikundi mbalimbali vya wakulima Afisa Kilimo aliomba kufuatilia vikundi ambavyo vipo ndani ya Halmashauri ya Ushetu, vilikabidhiwa *"power tiller"* na kuwasilisha majina ya vikundi hivyo vya wakulima mahali vilipo katika Mkutano wa Baraza.

Utekelezaji; Taarifa ya vikundi vya wakulima vilivyokabidhiwa power tiller iliambatanishwa.

Baada ya majibu ya utekelezaji kuwasilishwa Mhe. Ester Matone alitaka kujua *"power tiller"* mbili zilizobaki Halmashauri kwa ajili ya kutolea mafunzo.

Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika alieleza kuwa taarifa aliyotoa inaonesha *"power tiller"* zote na mahali zilipo Halmashauri haikubaki na power tiller hata moja.

MUHT NA. BM/43/2017/2018 - TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA MWEZI DISEMBA, 2017

Afisa Biashara aliwasilisha taarifa hiyo na kueleza kuwa kwa kipindi cha mwezi Desemba, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ilikusanya na kupokea jumla ya Tshs 2,114,055,327.59 na kutumia jumla ya Tshs 1,732,117,082.10 kutoka mapato ya ndani na ruzuku toka Serikali kuu kama ifuatavyo;

MAPATO	**Makisio 2017/2018 sh.**	**Mwezi Desemba2017**	**Mwezi Julai-Desemba2017**	**Albaki**	**Ufanisi %**
Mapato ya Ndani	2,697,998,000.00	438,294,927.59	1,563,588,184.09	1,134,409,815.91	58
Ruzuku za idara OC & GPG	912,758,000.00		407,000,200.00	505,757,800.00	45
Mshahara(PE)	17,236,060,000.00	1,140,018,000.00	6,802,307,800.00	10,433,752,200.00	33

Miradi ya Maendeleo	7,962,350,849.00	535,742,400.00	1,862,963,228.64	6,099,387,620.36	23
Jumla	28,809,166,849.00	2,114,055,327.59	10,635,859,412.73	18,173,307,436.27	37
MATUMIZI	**Makisio ya Mwaka 2017/2018.**	**Desemba2017/2018**	**Julai-Desemba 2017/2018**	**Albaki**	**Ufanisi%**
Mapato ya Ndani	947,599,200.00	69,707,927.07	546,419,672.34	41,179,527.66	58
Ruzuku za Idara	912,758,000.00	16,036,000.00	256,800,700.00	655,957,300.00	28
Mishahara (PE)	17,236,060,000.00	1,140,018,000.00	6,802,307,800	10,433,752,200	39
Wanawake na vijana	236,899,800.00		20,000,000.00	216,899,800.00	8
Maendeleo Mapato ya ndani	1,184,499,000.00	1,190,000	548,501,613	635,997,387	46
CHF, NHIF & PAPO KWA PAPO	325,000,000.00			325,000,000.00	0
Fedha toka serikali kuu & Wafadhili	7,962,350,849.00	505,165,155.03	1,344,992,915.32	6,617,357,933.68	17
Jumla	28,805,166,849.00	1,732,117,0882.10	8,449,816,731.35	20,355,350,117.65	29

Baada ya kuwasillisha taarifa hiyo wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Doa Limbu alipongeza ukusanyaji wa mapato na kueleza kuwa Halmashauri imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kuwawezesha wanawake na vijana alitaka kujua tangu imeanza kutoa fedha hizo ni kiasi gani ambacho kimesha rejeshwa.

Pia alitoa ushauri kuwa, kutokana na mapato ya Halmashauri kushuka kwa sababu ya punguzo la 2% katika zao la Tumbaku na Pamba aliomba Idara ya Ardhi iongeze juhudi katika ukusanyaji wa mapato kwa kuwa Halmashauri ilishanunua "*Total station*" na imeweka bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya upimaji yaani RTK.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa fedha zinazorejeshwa kupitia marejesho ya mikopo ya wanawake na vijana zinaingizwa kwenye akaunti ya amana na hadi sasa kiasi cha fedha kilichopo ni Shs. 34,000,000.

Kuhusu suala la ukusanyaji mapato Idara ya Ardhi ushauri ulipokelewa.

MUHT NA. BM/44/2017/2018 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI NGAZI YA KATA

Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kata za Ulowa, Bukomela, Ukune, Igwamanoni, Ulewe, Idahina, Mapamba, Nyamilangano na Bulungwa ziliwasilishwa na madiwani wa Kata husika.

MUHT NA. BM/45/2017/2018 – KUSITISHA MKUTANO WA BARAZA SIKU YA KWANZA

Katibu aliwapongeza wajumbe kwa majadiliano ya agenda za Mkutano siku ya kwanza kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kusitisha Mkutano.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuchakata ajenda za siku ya kwanza na kukamilisha. Aliomba masuala yote yaliyoshauriwa na wajumbe yapokelewe kwa ajili ya utekelezaji na yanayostahili kuwasilishwa katika vikao vya Kamati vinavyofuata yawasilishwe.
Alisitisha kikao 08: 27 Mchana.

MUHT NA. BM/46/2017/2018 – KUREJESHA MKUTANO WA BARAZA SIKU YA PILI

Katibu aliwakaribisha wajumbe, wataalam, wageni waalikwa na Waandishi wa Habari katika mkutano huo. Alieleza kuwa hakuweza kuhudhuria Mkutano huo siku ya kwanza kwa kuwa alikuwa safari ya kikazi ikiwa ni pamoja na kufuatilia kibali cha ununuzi wa gari la Idara ya Kilimo na Ushirika kutoka kwa Katibu Mkuu TAMISEMI, aliendelea kueleza kuwa katika safari hiyo alifanikiwa kufika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambapo alifanikiwa kupata watumishi wawili mmoja akiwa ni mtumishi Idara ya Kilimo na mwingine ni Mhandisi wa Ujenzi. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufungua kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, wataalam, wageni waalikwa na Waandishi wa Habari katika mkutano huo na kueleza kuwa Mkutano huo ni mwendelezo wa siku ya kwanza Kisha alifungua Kikao 5: 35 Asubuhi.

MUHT NA. BM/47/2017/2018 - MASWALI YA PAPO KWA PAPO
Mwenyekiti alieleza kuwa hadi mkutano huo unaanza alikuwa hajapokea swali lolote la papo kwa papo. Hivyo aliruhusu ajenda zingine ziendelee.

MUHT NA. BM/48/2017/2018 - TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO

Kaimu Afisa Mipango aliwasilisha taarifa hiyo, alieleza kuwa Halmashauri ina jumla ya miradi 178 yenye Bajeti ya Shilingi 5,716,467,605. Hadi mwisho wa robo ya pili, Halmashauri ilishapokea Fedha kiasi cha Shilingi 1,409,169,063 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Matumizi kwenye Miradi ni Shilingi 411,254,233.

Aliendelea kueleza na kufafanua miradi kadhaa iliyopokea fedha ikiwa ni pamoja na:

- ujenzi wa makao makuu

- miradi ya mapato ya ndani
- usambazaji wa maji vijijini
- mfuko wa jimbo
- Sekta ya afya Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi 400,000,000 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika kituo cha afya Ukune.

Baada ya taarifa hiyo iliyokuwa na viambatanisho na ufafanuzi kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:

(i) Kuhusu matengenezo ya Barabara

Mhe. Esther Matone alieleza kuwa barabara ya Nyalwelwe-Ulewe ni mbovu sana na Magari hayapiti katika maeneo hayo, hali inayopelekea kutishia maisha ya wananchi hasa kina mama wajawazito na wagonjwa wengine wanapokuwa wanaenda Hospitali. Aliomba mafuta yaliyobaki Halmashauri kwa ajili ya matengenezo ya Barabara wayakabidhi TARURA na waelekezwe kwenda kutengeneza barabara hiyo.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mhe. Doa Limbu, alitoa ushauri kuwa fedha iliyowekwa kwenye bajeti kwa ajili ya kutengeneza barabara kilometa 47.9 itakapopatikana ipelekwe TARURA kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na wapewe mitambo kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara zilizoharibika.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa anaelewa changamoto ya barabara za Halmashauri maeneo mengi ni mabovu, hata hivyo tayari kulikuwa na kikao ambacho kilifanyika kati ya Mkurugenzi na Naibu waziri pamoja na Meneja TARURA kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo na zingine ambazo zimeharibika. Alisema kuwa eneo la Nyalwelwe lina changamoto ambayo inapelekea hadi kutokea vifo vya wajawazito na tayari alishaomba fedha wizara ya afya kwa ajili ya kujenga zahanati katika kata hiyo.

Hata hivyo aliongeza kuwa bajeti inaanza kwa kuwekwa kwenye mpango na hatimaye ukusanyaji wa mapato unafuatia, hivyo ukusanyaji wa mapato ndio utakaofanya utekelezaji wa mikakati na mipango iliyopangwa, fedha za utengenezaji wa barabara ni fedha inayoletwa kutoka serikali kuu na robo inayofuata itatolewa taarifa kama utekelezaji utafanyika na fedha imepatikana kutoka wapi.

(ii) Kuhusu ununuzi wa gari la Idara ya Kilimo na Ushirika

Mhe. Doa Limbu alieleza kuwa katika mpango wa ununuzi wa gari la Idara ya Kilimo ilibajetiwa Tshs. 142,988,128 na katika mapokezi inaonesha Tsh. 165,000,000 alitaka kujua sababu iliyopelekea kuongezeka kwa fedha hizo.

Mkuregenzi Mtendaji alieleza kuwa fedha ya ununuzi wa gari la Idara ya Kilimo imeongezeka kutokana na mfumuko wa bei ambapo dola imepanda na kupelekea ongezeko la fedha hizo.

(iii) Kuhusu fedha za maendeleo asilimia 60 kupelekwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo

Mhe. Doa Limbu alieleza kuwa fedha za miradi ya maendeleo 60% ni fedha ambazo zinatakiwa kupelekwa kwenye miradi kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo na fedha hizo hazitolewi kama inavyotakiwa.

Mkuregenzi Mtendaji alieleza kuwa katika asilimia 60 kuna 10% ambazo ni fedha za wanawake, vijana na walemavu, 20% ni fedha ya Mifugo ambayo 15% inaenda katika Mifugo na 5% inaenda katika Uvuvi na hatimaye fedha inayobaki ndiyo inayopelekwa katika miradi ya maendeleo, hata hivyo fedha ambayo tayari ilishapelekwa katika miradi ya maendeleo imezidi asilimia zilizobaki.

(iv) kuhusu fedha za mfuko wa jimbo

Mhe. Sharifu Samwel alieleza kuwa fedha za mfuko wa jimbo hutolewa kwa ajili ya kuchochea maendeleo katika ngazi ya kata na vijiji lakini zimekuwa hazitolewi mapema hivyo alitaka kujua ni kwa nini fedha hizo zinapoidhinishwa zinachelewa kufika katika akaunti ya Kata au vijiji husika kwa ajili ya utekelezaji.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa, upelekaji wa fedha za miradi itategemea upatikanaji wa fedha. Lakini pia changamoto zingine zinazokwamisha kupeleka fedha mapema ni masuala ya kimtandao na wakati mwingine fedha haziingii kwa sababu akaunti zinakuwa hazijahuwishwa.

(v) Kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa Shule za sekondari

Mhe. Hamis Majogoro alieleza kuwa mikakati ya Halmashauri ilikuwa ni kukamilisha ujenzi wa Sekondari tatu ambazo ni Igunda, Nyankende na Sabasabini na baada ya Sekondari hizo kukamilika zitajengwa shule zingine ambazo ni Mapamba, Ubagwe na Bukomela, alitaka kujua utekelezaji wa kukamilisha shule hizo kwa lengo la kusaidia wananchi wa maeneo husika utakamilika lini.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa taarifa inayojadiliwa ni ya kipindi cha robo ya pili lakini kama fedha zitapatikana kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huo zitapelekwa mapema kwa ajili ya kufanya utekelezaji.

MUHT NA. BM/49/2017/2018 - TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI, OKTOBA HADI DESEMBA, 2017

Taarifa hizo ziliwasilishwa na wenyeviti wa kamati husika kama ifuatavyo:

1. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati wa kudhibiti UKIMWI Mhe. Gagi Lala Gagi, aliwasilisha taarifa ya utekelezaji ya kamati hiyo, iliyowasilishwa katika kikao cha kawaida cha Kamati ya kudhibiti UKIMWI cha tarehe 18/10/2017 ambapo muhtasari wake ulithibitishwa tarehe 25/01/2018 pamoja na taarifa ya utekelezaji katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba hadi Desemba) za kamati mseto ya kudhibiti UKIMWI zilizowasilishwa kwenye kikao cha kawaida cha tarehe 25/01/2018.

Mambo muhimu yaliyokuwa katika taarifa hiyo ni pamoja na;

A) MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 18/10/2017 NA MUHTASARI WAKE KUTHIBITISHWA TAREHE 25/01/2017

MUHT. NA. UK/6/2017/2018 - YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI CHA TAREHE 18/10/2017

Majibu ya utekelezaji wa yatokanayo yaliwasilishwa kama ifuatavyo:

Muht. Na. UK/10/2017/2018 – Kuhusu kuandika barua za shukrani kwa wafadhili kuonesha kutambua mchango wao

Azimio kwamba; Halmashauri iandae barua za shukrani kwa ajili ya kutambua michango mbalimbali ya wadau ambao wamekuwa wakifadhili ama kuwezesha shughuli za kudhibiti UKIMWI katika Halmashauri ya Ushetu.

Majibu ya utekelezaji yalitolewa kuwa; barua zilishaandikwa kwenda kwa wadau.

Baada ya majibu ya utekelezaji wajumbe wote kwa pamoja walipongeza kuwa ni jambo zuri kutambua mchango wa wadau kwa kuwaandikia barua

Uk/10/2017/2018 – Kuhusu kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kudhibiti UKIMWI robo ya pili

Azimio Kwamba: Halmashauri ihakikishe imetoa fedha kwa ajili ya shughuli za Kamati ya Kudhibiti UKIMWI zilizopangwa kutekelezwa kwa robo ya pili

Majibu ya utekelezaji yalitolewa kuwa: Malipo yameandaliwa shughuli zitatekelezwa robo inayofuata.

B) MUHT. NA. UK/8/2017/2018 – TATHIMINI YA ZIARA YA KUDHIBITI UKIMWI TAREHE IO/08/2017

Taarifa ya ziara ya kamati hiyo iliwasilishwa ikiwa na mjadala wa wajumbe.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KUDHIBITI UKIMWI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA HADI DESEMBA) 2017/2018

Ilielezwa kuwa katika kipindi cha robo ya pili, Halmashauri kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa huduma za kukabiliana na VVU/UKIMWI ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI, huduma za wagonjwa majumbani, ushauri nasaha na upimaji VVU kwa hiari na huduma ya bure ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Juhudi hizo zinalenga kufikia malengo ya sifuri tatu **''Maambukizi Mapya sifuri, Unyanyapaa na Ubaguzi Sifuri na Vifo Vitokanavyo na UKIMWI Sifuri''**

Baada ya taarifa ya kamati kuwasilishwa Mhe. Yohana Mange alishauri ziangaliwe zahanati ambazo zina maeneo yanayoweza kuwekewa CTC ili ziongezwe.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa masuala ya huduma za afya bajeti zake zinatengenezwa na wahusika katika vituo vyao na kisha zinapelekwa Wizara ya Afya na fedha zitaingizwa moja kwa moja katika vituo. Alishauri yale yote yanayohitajika

kwenye zahanati hizo waheshimiwa Madiwani waende kushauri katika vikao vya WDC ili yaingizwe kwenye bajeti.

2. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa kamati Mhe. Paschal N. Mayengo aliwasilisha taarifa ya Kamati kwa kuzingatia taarifa za utekelezaji za kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Desemba, 2017 na muhtasari wa kikao cha tarehe 20/10/2017 uliothibitishwa katika kikao cha tarehe 26/01/2018

Mambo muhimu yaliyokuwa katika taarifa hiyo ni pamoja na:

A) TAARIFA YA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MWEZI OKTOBA KILICHOFANYIKA TAREHE 20/10/2017

MUHT.NA. UUM/13/2017/2018 – YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 25/07/2017

Kutoka Muht. Na. UUM/07/2017/2018 Kuhusu Kilimo cha mkataba wa zao la Pamba

Azimio kwamba:- Kilimo cha mkataba kianzishwe kwa ushirika kama ilivyo vikundi vya wakulima wa Tumbaku. Aidha, mkataba huo uwe na manufaa kwa pande zote mbili

Utekelezaji, Usajili wa wakulima wa Pamba utafanyika kwa kila kitongoji/vijiji na maeneo yanayolimwa (Idadi ya Ekari) ili kupata mahitaji halisi ya pembejeo na matarajio ya mavuno. Pia rasimu ya mkataba imeandaliwa na kupitiwa na wanasheria wa Halmashauri zote tatu (3) ili kuhakikisha mkataba unakuwa na manufaa kwa pande zote.

B) MUHT.NA. UUM/14/2017/2018 – TATHMINI YA ZIARA YA KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA KUTEMBELEA MSITU WA USUMBWA TAREHE 11/08/2017

Taarifa iliwasilishwa na Afisa Ardhi na maliasili ambapo ziara ilifanyika katika maeneo matatu ambayo ni;

1. Bwawa la Ngara
2. Msitu wa Ushetu/ Ubagwe
3. Msitu wa Usumbwa

taarifa hiyo ilikuwa na maoni pamoja na ushauri wa wajumbe wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.

C) TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA - DESEMBA), 2017/2018

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri ya Wilaya katika kipindi chote cha robo ya pili (Oktoba hadi Desemba) 2017/2018 za Idara na Vitengo vya kamati pamoja na Taarifa ya uendeshaji wa mitambo ya Halmashauri kwa kipindi cha robo ya pili zikiwa zimeambatanishwa.

Baada ya taarifa ya kamati kuwasilishwa Mhe. Kulwa Shoto alieleza kuwa Idara ya Kilimo na Ushirika bado kuna changamoto ya Pembejeo za kilimo, hali inayopelekea wakulima kukosa Pembejeo mapema na pindi zinapopatikana bei inakuwa ni kubwa, hivyo alitoa ushauri kwa Idara hiyo kufuatilia na kujua sababu inayopelekea pembejeo kuchelewa ili kusaidia wakulima.

Ushauri ulipokelewa.

3. KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI

Mwenyekiti wa kamati hiyo Mheshimiwa Tabu R.Katoto aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji kwa kuzingatia taarifa za kikao na muhtasari uliothibitishwa kwa kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Desemba, 2017. Kikao hicho ni Kikao cha kawaida cha mwezi Oktoba cha kamati ya Elimu, Afya na Maji kilichofanyika tarehe 19/10/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 26/01/2018

Mambo muhimu yaliyowasilishwa ilikuwa ni:

A) KIKAO CHA KAWAIDA CHA MWEZI JULAI KILICHOFANYIKA TAREHE 19/10/2017

Kamati ya Elimu katika kikao cha kawaida ilijadili na kupokea taarifa mbalimbali kama ifuatavyo

MUHT.NA.EAM/04/2017/2018 – YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA ELIMU AFYA NA MAJI CHA TAREHE 24/07/2017

Kutoka Muht. Na. EAM/32/2016/2017 – Kuhusu wajumbe wa kamati ya Mikopo ya Wilaya.

Azimio kwamba ; Ofisi ya Mkurugenzi iwasilishe;

1. Mwongozo uliopo wa uundaji wa Kamati ya Mikopo ya Wilaya
2. Majina, vikundi na kata wanazotoka wajumbe wawili ambao ni wawakilishi wa wanawake na vikundi vya wajasiliamali
3. Rasimu ya mwongozo wa wajumbe wa Kamati ya Mikopo ya Wilaya

Utekelezaji

1. Miongozo imeambatanishwa
2. Majina ya wawakilishi
   i) Christina Ramadhani kutoka kata ya Igwamanoni kikundi cha mwendapole
   ii) Ajira Richard kutoka kata ya Ulewe kikundi cha Agape
   iii) Rasimu ya Mwongozo wa uendeshaji wa mfuko wa maendeleo ya wanawake (WDF) umeambatanishwa.

B) MUHT.NA.EAM/12/2017/2018 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI SHUGHULI ZA HALMASHAURI YA WILAYA ROBO YA KWANZA (JULAI HADI SEPTEMBA) 2017/2018 ZA IDARA ZA KAMATI

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri ya Wilaya katika kipindi chote cha robo ya pili (Oktoba hadi Desemba) 2017/2018 za Idara na Vitengo zikiwa zimeambatanishwa.

Baada ya taarifa hizo kuwasilishwa wajumbe walijadili masuala mbalimbali kama ifuatavyo;

(i) Kuhusu mradi wa maji wa visima virefu

Mhe. Sharifu Samwel alitaka kujua kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji wa visima virefu ni vingapi vilivyochimbwa vimepata maji ya kutosha na vingapi havina maji ya kutosha, gharama zake pamoja na mkataba wa uchimbaji.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mhe. Pili Sonje, alishauri maeneo yaliyokosa maji utafiti urudiwe na kama itaonekana bado hayatoshi kazi ya kuchimba visima kwa maeneo hayo ifanyike mapema. Aidha, aliomba katika orodha ya visima vya maji vitakavyochimbwa kwa upande wa Kata ya Ushetu ibadilishwe kutoka Mkwangulwa kwenda Mhuge.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa ushauri wa mheshimiwa diwani umepokelewa, katika makubaliano ya mkataba wa kazi na Mkandarasi ilikuwa ni kufanya utafiti, kuchimba na kufanya vipimo vya wingi wa maji hadi maji yatakapopatikana ya kutosha vinginevyo mkataba wake hauruhusu kulipwa. Aliongeza kuwa visima vilivyochimbwa na kupata maji na vyenye maji pungufu taarifa za msingi zenye usahihi zitapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

(ii) kuhusu mikopo ya Wanawake, vijana na walemavu

Mhe. Sharifu Samwel alieleza kuwa waheshimiwa madiwani waliwahi kushauri fedha za mfuko huo ziwe na akaunti inayojitegemea ili fedha hizo ziwe na utaratibu mzuri wa kutumika. Aidha alitaka kujua ni vikundi vingapi viliomba mkopo, vilivyopata na vilivyokosa na fedha iliyopatikana kwa ajili ya kukopesha.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mhe. Doa Limbu alieleza kuwa vikundi vilivyopo ni 95 na kikundi cha walemavu ni kimoja alitaka kujua kuna changamoto gani inayokwamisha kuwafikia walemavu na kuwapa elimu ya kujiunga katika vikundi ili kuwakopesha.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa awali mfuko huo ulikuwa na akaunti iliyojitegemea baadaye Serikali iliona hakuna haja ya kuwa na akaunti nyingi na kuondoa baadhi na kubakiza akaunti sita (6). Aliongeza kuwa fedha za mfuko huo tayari mweka hazina alisha anzisha utaratibu wa kuzitunza ndani ya akaunti ya amana.

Aidha alieleza kuwa taarifa zilizopita zilionesha vikundi ambavyo vilishakopeshwa na fedha zilizoombwa sasa kwa ajili ya kukopesha ni 80,000,000 fedha ambayo itategemea ukusanyaji wa mapato.

Pia alieleza kuhusu suala la kutoa elimu juu ya mikopo kuwa inatolewa, changamoto ni wananchi wanapohitaji kupewa mikopo bila kuwa na miradi wanayoendesha hivyo kufanya vikundi kukosa sifa. Katika uhamasishaji aliongeza kuwa upande wa walemavu iliandaliwa barua ambayo ilipelekwa katika chama cha walemavu na kikundi kilichojitokeza ni cha chambo na kilipata fedha hizo na kuna kikundi ambacho kilileta maombi kutoka Igunda. Alisisitiza kuwa fedha itakayopatikana katika mapato ya ndani katika 60% zitatengwa 10% kwa ajili ya Wanawake, Vijana na Walemavu.

4. KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO

Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Gagi Lala Gagi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango aliwasilisha taarifa ya kamati. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa kuzingatia taarifa za vikao na mihtasari iliyothibitishwa kwa kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Desemba, 2017/2018. Vikao hivyo ni:

A. Kikao cha kawaida cha mwezi Oktoba cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 26/10/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 17/11/2017
B. kikao cha robo ya kwanza (Julai – Septemba) cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 30/10/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 06/02/2018
C. Kikao cha kawaida cha mwezi Novemba cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 17/11/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 15/12/2017
D. Kikao cha kawaida cha mwezi Desemba cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 15/12/2017 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 29/01/2018.

(I) MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI

A. MAPATO

Ilielezwa kuwa kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2017/2018 Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya shilingi 10,635,859,412.73 Shilingi 1,563,588,184.09 ni fedha za mapato ya ndani sawa na asilimia 58 ya lengo la mwaka 2017/2018 la makisio ya shilingi 2,697,998,000.00

B. MATUMIZI

Ilielezwa kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2017/2018, Halmashauri ilitumia jumla ya shilingi 8,449,816,731.35 ambapo kati ya hizo shilingi 1,094,921,285.03 ni fedha za makusanyo ya ndani, hivyo kufanya matumizi kwa mapato ya ndani kuwa asilimia 40.6

(II) VIKAO

A. KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 26/10/2017

Kamati ya Fedha katika kikao cha kawaida ilijadili na kupokea taarifa mbalimbali kama ifuatavyo

MUHT. NA. FUM/51/2017/2018 - TAARIFA MBALIMBALI ZA KIUTUMISHI KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2017

Ilielezwa kuwa Idara ya Utumishi inashughulikia masuala mbalimbali ya watumishi ikiwa ni pamoja na kuajiri, kupandisha madaraja watumishi wenye sifa, kuthibitisha kazini watumishi waliokidhi vigezo vya kuthibitishwa kazini na masuala yote ya kiutumishi kama vile kusimamia nidhamu ya watumishi na kusimamia wajibu na haki za watumishi wote.

katika kipindi cha mwezi Septemba, 2017 masuala mbalimbali ya kiutumishi yalijiri ikiwa ni pamoja na taarifa za utoro, taarifa za uhamisho n.k

Upande wa mishahara, kwa mwezi Septemba, 2017 Halmashauri ililipa kiasi cha Tsh.1, 131,591,350/= kwa watumishi 1786. Kati ya hao, watumishi 1,763 walilipwa Tsh. 1,126,208,000/= kwa Ruzuku toka Serikali kuu na watumishi 21 walilipwa Tsh. 5,383,350/= kwa ruzuku ya mapato ya ndani. Kati ya watumisi 23 watumishi 19 ni wa Mkataba na watumishi 04 ni ajira ya kudumu.

MUHT. NA. FUM/52/2017/2018 - TAARIFA YA BODI YA AJIRA

Ilielezwa kuwa Halmashauri ilipata kibali cha Ajira mpya tarehe 17 Julai, 2017 chenye kumb. Na.FA.170/376/01/57 na Ajira mbadala cha tarehe 22 Agosti, 2017 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika kibali hicho nafasi ambazo zilishughulikiwa na ngazi ya Halmashauri ni:

- Nafasi mbili za Dereva II
- Nafasi mbili za katibu muhtasi III
- Nafasi 33 za watendaji wa Vijiji

Utekelezaji wa vibali hivyo vya ajira ulifanyika.

B: KIKAO CHA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) CHA TAREHE 30/10/2017

Katika kikao cha robo ya kwanza kamati ilijadili na kupokea taarifa kama ifuatavyo:

MUHT. NA.FUM/56/2017/2018 - TAARIFA YA MWENENDO WA KESI ZA HALMASHAURI HADI KUFIKIA SEPTEMBA 30, 2017

Hadi kufikia tarehe 30/09/2017 kulikuwa na jumla ya kesi 4 ambazo zilihusisha Halmashauri, ambazo mbili ni za madai na 2 ni za ardhi.

MUHT. NA.FUM/57/2017/2018 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA MWAKA 2017/2018.

Taarifa hiyo iliwasilishwa ikiwa na sehemu mbili ambapo Sehemu A, ilielezea utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo na Sehemu B, ilielezea utekelezaji wa Miradi ya Bakaa.

MUHT. NA.FUM/58/2017/2018 - TAARIFA YA MANUNUZI YA BODI YA ZABUNI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI-SEPTEMBA) 2017/2018

Katika kipindi cha robo ya kwanza ilielezwa kuwa bodi ya zabuni ilifanya manunuzi ya shajala za Ofisi, mafuta ya magari na pikipiki, Ununuzi wa matairi ya magari na mitambo, matengenezo ya magari, ununuzi wa vifusi na vifaa vya maji vya ujenzi wa Ofisi ya muda makao makuu ya Halmashauri.

MUHT. NA. FUM/59/2017/2018 - TAARIFA YA HOJA ZA UKAGUZI

Taarifa iliwasilishwa ikiwa ni pamoja na majibu ya menejimenti na kufafanuliwa kuwa, taarifa ina jumla ya hoja saba 7 ambapo hoja 6.1 imejumuisha hoja za miaka ya nyuma za CAG na hoja namba 8.1.1, 8.2.1, 8.3.1.2 na 8.4.1 zilijitokeza katika kipindi cha robo ya kwanza.

MUHT. NA.FUM/61/2017/2018 - TATHMINI YA ZIARA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO TAREHE 23 – 24/10/2017

Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha na tathmini yake iliyofanyika tarehe 23-24/10/2017 ilihusisha miradi 12 iliyotembelewa.

C: KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 17/11/2017

Kamati ya Fedha katika kikao cha kawaida ilijadili na kupokea taarifa mbalimbali kama ifuatavyo

MUHT. NA. FUM/68/2017/2018 - TAARIFA MBALIMBALI ZA KIUTUMISHI KWA MWEZI OKTOBA, 2017

Masuala mbalimbali ya kiutumishi yaliyojiri katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2017 yalihusu uhamisho na Utoro kazini kwa watumishi.

Kuhusu mishahara ilielezwa kuwa, kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2017 Halmashauri ilifanikiwa kulipa mishahara kiasi cha Tsh.1,130,470 ,350/= kwa watumishi 1,783 kati ya hao, watumishi 1,760 wamelipwa Tsh 1,126,208,000/= kwa Ruzuku toka Serikali kuu na watumishi 21 wamelipwa Tsh 5,383,350/= kwa ruzuku ya mapato ya ndani. Kati ya watumishi 23 watumishi 19 ni wa mkataba na watumishi 04 ni ajira ya kudumu kupitia Mapato ya ndani.

MAOMBI YA KIBALI CHA WAKUU WA IDARA KUIDHINISHA MALIPO KWENYE HATI ZA MALIPO (PAYMENT VOUCHERS)

Iliwasilishwa taarifa ya kuomba kuidhinishiwa majina ya wakuu wa Idara watakao idhinisha malipo kwenye hati za malipo (payment vouchers). Ilielezwa kuwa mwongozo wa Serikali kupitia Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wakati Serikali ilipoanzisha akaunti sita (6) za malipo ya Serikali katika Mamlaka ya Serikali za mitaa wa tarehe wa 30 April 2012; uliagiza kuwa Afisa Masuuli au Afisa aliyeteuliwa na Afisa masuuli na kupitishwa na Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango ndiye atakayekuwa na dhamana ya kuidhinisha malipo kwenye hati za malipo (payment vouchers) mbalimbali za Halmashauri.

Kwa kuzingatia matakwa hayo ya kisheria Mkurugenzi Mtendaji aliomba majina hayo yaidhinishwe, ili watakapokuwa wamekaimishwa majukumu ya kiutendaji ya Mkurugenzi Mtendaji waidhinishe vocha za malipo.

Majina hayo yalikuwa kama yalivyooneshwa kwenye jedwali:

NA	JINA	CHEO
1	Pambe Charles Pambe	Mkuu wa Idara ya Maji
2	Sadick Joseph Mwita	Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
3	Onesmo Benjamini Bwakea	Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
4	Anna Marco Ngongi	Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji
5	Athanas Machiya Lucas	Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
6	Marco Selestini Mwairwa	Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili

Wajumbe waliafiki maombi hayo na kuagiza utekelezaji uanze kufanyika.

MUHT. NA. FUM/74/2017/2018 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA JENGO LA UTAWALA MAKAO MAKUU – NYAMILANGANO

Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ilipokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na 2016/2017. Kupitia Baraza la Madiwani zilipitishwa Shs 300,000,000.00 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo.

Aidha, Pamoja na ujenzi wa jengo hilo, kuna mkakati unaoendelea wa kujenga jengo la ghorofa mbili ili kukidhi mahitaji halisi ya Halmashauri.

Baada ya kuwasilisha taaarifa hiyo wajumbe kwa pamoja waliridhia gharama zilizotumika kwa kuzingatia thamani ya fedha na ubora uliotumika kwenye ujenzi wa jengo kuwa ni sahihi na taarifa hiyo ilipokelewa.

D: KIKAO CHA KAWAIDA CHA TAREHE 15/12/2017

Kamati ya Fedha katika kikao cha kawaida ilijadili na kupokea taarifa mbalimbali kama ifuatavyo

MUHT.NA. FUM/82/2017/2018 - MAPENDEKEZO YA KUFANYA MABADILIKO YA VIFUNGU VYA BAJETI (BUDGET REALLOCATIAN)

Halmashauri iliendelea na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017 – 2018, kutokana na mahitaji kubadilika wakati wa utekelezaji ilipelekea kuwepo umuhimu wa kufanya mabadiliko ya vifungu vya bajeti (budget reallocation) kama sheria ya bajeti ya mwaka 2015 sehemu ya 41 inavyoelekeza.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliafiki maombi hayo na kuagiza utekelezaji wa kupata kibali cha kufanya mabadiliko uendelee ili shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa zikamilishwe.

MUHT.NA. FUM/83/2017/2018 – MAPENDEKEZO YA KUBADILI WAWEKA SAINI KATIKA AKAUNTI ZA HALMASHAURI

Taarifa hiyo ya kuomba idhini ya kubadilisha watia saini katika akaunti za Halmashauri kutokana na watumishi waliokuwa watia sahihi katika Akaunti za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kupata Uhamisho wa kwenda Halmashauri

nyingine iliwasilishwa. Watumishi hao waliokuwa waweka saini ni mkuu wa Idara ya Maji, Idara ya Fedha na Afya.

MUHT.NA. FUM/85/2017/2018 – MAPENDEKEZO YA KUFUTA VITABU

Ilielezwa kuwa mwongozo wa uhasibu wa Mamlaka za Serikali za mitaa "Local Authority Accounting Manual" wa mwaka 2010 kifungu cha 5.9 na kanuni za fedha za mamlaka za Serikali za Mitaa "Local Authority Financial Memorandum" ya mwaka 2009 kifungu 63 (3) kinamtaka Afisa Masuuli pale inapotokea upotevu wa vitabu vya kukusanyia fedha atoe taarifa kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na nakala ipelekwe kwa Mkuu wa Mkoa.

Alieleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya vitabu tisa (09) vyenye namba zilizooneshwa hapo chini vilipotea;

Namba	**Idadi**	**Jina la aliyekuwa nacho**	**Cheo**
31751 - 31800	1	Nehemia G. Kyando	WEO Mpunze
54601 – 54650	1	Yohana E. Mpemba	WEO Ushetu
54801 - 54850	1	Yohana E. Mpemba	WEO Ushetu
55001 - 55050	1	Yohana E. Mpemba	WEO Ushetu
55501 - 55550	1	Michael P. Nzani	WEO Igunda
55601 - 55650	1	Michael P. Nzani	WEO Igunda
56551 - 56600	1	Michael P. Nzani	WEO Igunda
57101 - 57150	1	Yohana E. Mpemba	WEO Ushetu
57751 - 57800	1	Paul L. Nguwa	WEO Nyankende
Jumla	**9**		

Baada ya kuwasilisha taaarifa hiyo wajumbe kwa pamoja waliridhia na kuunga mkono suala la kufuta vitabu hivyo vilivyopotea.

MUHT.NA. FUM/86/2017/2018 –PENDEKEZO LA FEDHA ZA MATUMIZI MADOGO MADOGO (STANDING IMPREST)

Ilielezwa kuwa sheria ya fedha za Serikali za Mitaa "Local Authority Financial Memorandum" ya mwaka 2009 (na marekebisho yake) kifungu cha 39 kinatoa mamlaka kwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kuweka kiwango cha fedha ya matumizi madogo madogo na dharura ya ofisi kitakachokuwepo wakati wote "Standing Imprest". Hivyo kwa mujibu wa sheria tajwa hapo juu aliomba kuwasilisha mapendekezo ya Tshs 5,000,000 kwa matumizi tajwa.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliridhia mapendekezo ya fedha hizo.

MUHT.NA. FUM/87/2017/2018 – TAARIFA MBALIMBALI ZA KIUTUMISHI KWA MWEZI NOVEMBA, 2017

Iliwasilishwa taarifa ya masuala mbalimbali ya kiutumishi yaliyojiri katika kipindi cha mwezi Novemba, 2017 ambayo yalihusu ajira mpya, ukomo wa ajira, uhamisho na utoro kazini.

Kuhusu mishahara ilielezwa kuwa, kwa kipindi cha mwezi Novemba, 2017 Halmashauri ilifanikiwa kulipa mishahara kiasi cha Tsh.1,130,270 ,350/= kwa watumishi 1,781 kati ya hao, watumishi 1,759 wamelipwa Tsh 1,126,208,000/= kwa Ruzuku toka Serikali kuu na watumishi 22 walilipwa Tsh 5,183,350/= kwa ruzuku ya

mapato ya ndani. Kati ya watumishi 22 watumishi 18 ni wa mkataba na watumishi 04 ni ajira ya kudumu.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliipokea.

MUHT.NA. FUM/90/2017/2018 – TAARIFA YA KUKABIDHI RASMI MAJENGO YALIYOKUWA YAKITUMIWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU YALIYOPO MJINI KAHAMA

Taarifa hiyo iliwasilishwa na kueleza kuwa, mnamo tarehe 30/11/2017 Halmashauri ya Ushetu ilipata ugeni wa Naibu waziri wa TAMISEMI Mhe. Joseph George Kakunda (MB) ambaye aliitisha kikao cha ndani tarehe 30/11/2017 kuhudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ushetu, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu na kuwaeleza kuwa moja ya mambo ya kufanya katika ziara yake wilaya ya Kahama ni pamoja na kutekeleza agizo la Rais la kusimamia makabidhiano ya majengo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwenda Halmashauri ya Kahama Mji.

Tarehe 01/12/2017 Naibu waziri, Mkurugenzi wa Ushetu na Halmashauri ya Mji Kahama walifanya makabidhiano ya majengo kwa kukabidhi funguo zote za majengo hayo kwa Naibu Waziri mbele ya waandishi wa Habari. Naye alimkabidhi Mkurugenzi wa Mji Kahama.

Katika kukabidhi majengo hayo, Naibu Waziri alieleza kuwa, kwa kuwa majengo hayo yalijengwa na Serikali hayana budi kuendelea kufanya shughuli za kiserikali na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu itapewa fedha za kujenga majengo yake katika mamlaka yake ya utawala.

Wajumbe kwa pamoja walionesha masikitiko yao na kusisitiza kuwa hawajaridhika na makabidhiano yaliyofanyika ya majengo hayo, na kamati kuagiza kuwa taarifa hiyo iende hadi kwenye Baraza la Madiwani.

Baada ya taarifa ya kamati kuwasilishwa Mhe. Doa M. Limbu alitaka kujua kuhusu suala la umeme wa REA awamu ya III utafika lini katika maeneo ambayo yalikuwa yameainishwa kwa Halmashauri ya Ushetu.

Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa taarifa rasmi za umeme wa REA awamu ya III bado hajazipokea, hivyo hakuna majibu sahihi ambayo angeweza kuyatoa.

MUHT NA. BM/50/2017/2018 – KUFUNGA MKUTANO

Katibu alieleza kuwa kuna fomu ambazo waheshimiwa Madiwani walitakiwa kujaza kutokana na mfumo wa malipo umebadilishwa. Hivyo aliomba fomu hizo zijazwe kwa haraka ili kukamilisha mchakato huo na malipo yote ya Serikali yatakuwa yanatoka moja kwa moja Benki Kuu kwenda kwa muhusika.

Aliwashukuru Madiwani kwa mjadala waliochangia na kueleza kuwa yale yote yaliyoshauriwa ameyapokea na atayafanyia kazi. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani kwa kuchangia ajenda zilizowasilishwa siku ya pili lengo ikiwa ni kushauri na kuleta mafanikio katika Halmashauri.

Alifunga kikao saa 10:06 Jioni.

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA

NA

SAINI:	**SAINI: .....**
JINA:	**JINA: .....**
CHEO: KATIBU	**CHEO: MWENYEKITI**

.....
TAREHE